
CHRIS SPARKS

# Unyakuo wa Siri



Je, ni fundisho ya Biblia?

## UNYAKUO WA SIRI:
## JE, NI FUNDISHO YA BIBLIA?

Neno 'kunyakuliwa' linatokana na neno la Kilatini 'rapizo', ambalo linamaanisha kunyakua au unyakuo.

Wakristo wote wanaamini kwamba Bwana atarudi kuwachukua watu wake kwenda nao mbinguni. Lakini wale wanaoamini unyakuo wa kabla ya nyakati za dhiki, kama vile Mchungaji John Macarthur, wanaamini kuwa tukio hili litatokea kwa *siri*.

Madai yao ni kuwa Wakristo wataondolewa duniani bila ya wao wenyewe au watu wengine kupewa onyo la kujiandaa kunyakuliwa, na kuwaacha wale wote wasioamini wakibakia nyuma sana na kukumbana na kipindi cha miaka saba yenye misukosuko. Fikiria maelezo ya John MacArthur hapa chini:


> Itatokea kwa dakika moja, kufumba na kufumbua.…Kwa haraka sana Wakristo wote walio wa kweli watatoweka mara moja kwenye sayari hii.…Sasa hebu fikiria juu ya hili, jambo hilo likitokea, litakuwa ni gumu kwa watu wale waliobakia duniani, wakati Wakristo wote waliopo kwenye sayari yote wakitoweka kwa ghafla. Ndiyo, rubani na rubani mwenza. Ikiwa unasafiri kwa ndege hiyo, huo utakuwa ndiyo mwisho.…Ni tukio lisilo na ishara. Linaweza kutokea wakati wowote. Hakuna kitu cha kinabii kinachohitajika kufanyika kabla haya hayajatokea.

Kulingana na theolojia hii, kunyakuliwa kwa waumini ni tukio la tofauti na ujio wa pili wa Kristo. John Macarthur anauelezea mwenendo wa matukio kama ifuatavyo:

> Itakuwa ni unyakuo wa kanisa. Hilo ni tukio ambalo halina ishara ya kutokea. Kwa maneno mengine, hakuna ishara ya utangulizi wa kutokea kwa tukio hilo. Itakuwa ni kwa ghafla—kwa muda mfupi, yaani kufumba na kufumbua—kulinyakua kanisa. Kisha kutakuwa na kipindi cha miaka saba yenye dhiki. Danieli anarejelea kipindi hicho na kipindi hicho kimeandikwa kwenye kitabu cha Ufunuo

kwa kujirudia rudia. Na hata namba zimewekwa. Na nilisema hiyo itafuatiwa na kurudi kwa Yesu Kristo kuanzisha ufalme Wake wa miaka elfu....Na mwisho wa ile miaka elfu, Shetani anafanya uasi. Hapo uasi wa Shetani unakuwa umekwisha. Na kisha ulimwengu wote kama tunavyoujua unapatwa na mlipuko wa atomiki na Bwana anaiumba mbingu mpya na dunia mpya.

Kwa ufanisi, wanaoamini unyakuo wa kabla ya dhiki wanaamini kuwa kuna ujio wa pili wa aina mbili. Ujio mmoja wa siri wa pili kwa waaminio, na ujio *wa pili* unaofuatia utashuhudiwa na wote watakaokuwa hai baada ya dhiki ya miaka saba kupita.




Hata hivyo, hakuna mahali ambapo Biblia inazungumza juu ya ujio wa pili wa aina mbili. John Macarthur anabishia kuhusu utengano wa unyakuo na ujio wa pili kwa kiasi kikubwa kwa sababu ungewaepusha waamini kupitia mateso.

Tena turudi kwenye Yohana 14, Yesu aliwaambia wanafunzi wake: 'Naenda kuwaandalia mahali. Nitakuja tena niwakaribishe kwangu'. Hakusema: 'Oh, lakini kabla sijafanya hivyo, mtapitia hukumu ya kutisha'. Alisema tu: 'Nisubirini. Nitarudi'. Walielewa kuwa Alimaanisha kuwaokoa kutoka kwenye ghadhabu inayokuja! Kwa hiyo huu ndio msingi thabiti, wenye nguvu wa tukio hili tukufu.

Je, Neno la Mungu linatuhakikishia kuwa mateso yataepukika? Hakika sivyo ilivyo. Kinyume chake ni kuwa dhiki, pamoja na uhakika wa amani, ndio hasa Bwana aliwaahidi watu Wake:

> Yohana 16:33 Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu.

Wanafunzi waliitambua kiukamilifu ahadi hii wakati wa kupigwa mawe kwa Stefano na kisha baadaye ikawa ni kwa mmoja baada ya mwingine kuuawa. Kadri miaka ilivyosogea, idadi isiyohesabika ya mashujaa walipitia mateso makali vivyo hivyo. Na sisi tunaoishi kwenye zama za giza je tutarajie kiwango kidogo cha mateso ukilinganisha na hiki?

Biblia haikuandikwa kwa ajili ya mtu asiyeamini na asiyejali mambo. Iliandikwa kwa ajili ya wale wanaotamani kujua yatakayokuja mbeleni. Iliandikwa ili kuwatayarisha, si kwa ajili ya maisha ya raha, bali kwa ajili ya dhiki, mahangaiko, manyanyaso, njaa, kuachwa tukiwa uchi, hatari, na kupigwa kwa upanga. Hakika, Maandiko yanatangaza kuwa "naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa." Lakini katika hayo yote, ahadi ya Bwana wetu ni hii isemayo "na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."

Ingawa John Macarthur anatangaza kuwa sehemu kubwa ya Ufunuo hailihusu kanisa, yeye anasema kuwa "kila kitu kingine cha kwenye Agano Jipya kinaelekezwa kwenye kanisa":

> [Mbali na Kitabu cha Ufunuo] kila kitu kingine kwenye Agano Jipya kinaelekezwa kwenye kanisa. Kila waraka, mafundisho yote kwenye Agano Jipya yanaelekezwa kwenye kanisa.

Kisha kwenye mahubiri yale yale, anatoa madai ya kuudhi:

> …kukosekana kwa maagizo au onyo kwa kanisa kuhusu dhiki. Unafikiri kama tungepitia hayo, kungekuwa na maagizo kwenye Biblia kuhusu kile tunachopaswa kukitazamia. Lakini hakuna chochote. Siku zote ni za baraka. Daima tunaambiwa kuwa Kristo anakuja. Daima tunalo lile tumaini lenye baraka na ufunuo wa utukufu wa Kristo. Tunamtazamia Kristo, hatumtazamii mpinga Kristo.

Akizungumza juu ya siku kabla ya kuja Kwake, Bwana wetu alitabiri juu ya mambo mengi tunayopaswa kuyatarajia, na kulionya kanisa lake—wale wanaoiamini Biblia—wasijali pale waonapo maafa na mateso yakitokea:

> Marko 13:7 Nanyi mtakaposikia habari za vita na uvumi wa vita, msitishwe; hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado.
> 13:8 Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na matetemeko ya nchi mahali mahali; kutakuwako na njaa; hayo ndiyo mwanzo wa utungu.
> 13:9 Nanyi jihadharini nafsi zenu; maana watawapeleka ninyi mabarazani, na katika masinagogi mtapigwa; nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao....
> 13:12 Na ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe, na baba atamsaliti mtoto; na watoto watashambulia wazazi wao na kuwafisha....
> 13:19 Kwa maana siku hizi zitakuwa na dhiki, jinsi isivyokuwa tangu mwanzo wa kuumba alipoumba Mungu hata sasa, wala haitakuwa kamwe.
> 13:20 Na kama Bwana asingalizikatiza siku hizo, asingeokoka mtu yeyote; lakini kwa ajili ya wateule aliowateua amezikatiza siku hizo.

Baada ya kuyaorodhesha majaribu haya yote ambayo wateule wanayatarajia, Yesu anaelekeza kuwa wanapaswa kuyazingatia maneno yake:

> Marko 13:23 Bali ninyi jihadharini; nimekwisha kuwaonya yote mbele.

Hata hivyo, kulingana na theolojia ya kunyakuliwa kabla ya wakati wa dhiki, hakuna haja ya kutilia maanani onyo la kabla ya kurudi kwa Kristo, kwani kulingana na hayo, waamini wote watapelekwa kwenye sehemu salama kabla hata ya kuanza kwa nyakati za dhiki Alizozitabiri. Kama John MacArthur asemavyo:

> Unafikiri kama tungepitia hayo, kungekuwa na maagizo kwenye

> Biblia kuhusu kile tunachopaswa kukitazamia. Lakini hakuna chochote. Siku zote ni tumaini lililobarikiwa.

Mambo haya mapesi na nyororo ni ya unabii wenye kuhadaa, ambayo mamilioni ya watu wanaingizwa kwenye uamsho mbaya zaidi.

Ni lazima watu wa Mungu wavumilie mateso na hata kifo cha imani badala ya kunyakuliwa kabla ya wakati wa taabu kuja. Wanakuwa tayari kuchukiwa na watu wote waliofuata mambo ya ulimwenguni.

> Mathayo 24:9 Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua...

> Marko 13:13 Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusubiri hata mwisho, ndiye atakayeokoka.

Lakini hatimaye, watakatifu hawa wa kudumu watakombolewa kutoka kwenye mkono wa mdhalimu. Mtesaji atatazama juu kwa hofu wakati ambapo Mwana wa Mungu anashuka kutoka juu kwenye utukufu:

> Ufunuo 1:7 Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina.

Kunyakuliwa kwa mawindo matakatifu kutoka kwenye meno ya mwovu kutakuwa ni ya utukufu kweli kweli. Bado tukio hili la ushindi litapeperushwa na tukio tukufu zaidi: faida ya wafu kutoka makaburini mwao na utukufu wa kuinuliwa kwa watakatifu wote.

Wakati huu wa ushindi hautakuwa kwenye siri, lakini utaangaziwa vyema sana na sherehe. Kristo anaposhuka kuwafufua wafu na kuwapokea walio hai, anavitangaza viumbe vyote kushuhudia kutimia kwa ahadi yake kwa uthabiti:

> 1 Wathesalonike 4:16 Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu,

> na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza;
> 4:17 Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.

Akilitukuza tukio hilo kwa mlio wa sauti Yake kuu na mlio wa tarumbeta, kifungu hiki kinanukuliwa mara kwa mara kuhusu muungurumo wa ufufuo wa asili yake. Inashangaza ni jinsi gani mtu mwenye akili anavyoweza kuvisoma vifungu hivi na kusema kuwa ni kwa siri.

## DHANA POTOFU ZA KINABII

Ingawa dhana potovu ya unyakuo wa siri inatosha kusababisha mkanganyiko mkubwa na kutojitayarisha, kinachoifanya theolojia hii iwe mbaya zaidi ni ukweli kuwa unyakuo wa siri ndiyo msingi wa muundo mzima wa kutoelewa unabii wa siku za mwisho.

Somo la mpinga-Kristo ni mada inayoenea kwenye vitabu vya Danieli na Ufunuo. Kielelezo hiki kinasemwa kwenye mamia ya nyakati kwenye Maandiko.

Watu wa Mungu wanaonywa kuwa mpinga-Kristo atafanya vita dhidi ya watakatifu na kuwaua, kuwa ataudanganya ulimwengu ili kupokea alama yake, na kuwa ghadhabu ya Mungu itamwagwa juu ya wote wanaoangukia kwenye udanganyifu wake. Hata hivyo maonyo kama hayo hayana maana sana kwa watetezi wa masuala ya unyakuo wa kabla ya nyakati za dhiki, kama inavyooneshwa na wanatheolojia maarufu ikiwemo Dkt. Mark Hitchcock na Dkt. John Hull, ambao hawatili mkazo kutafuta utambulisho wa mpinga-Kristo:

> Hitchcock: Ninafikiri tayari Shetani huwa anaye mtu kwenye kila kizazi. Daima ninafikiri kuna mpinga-Kristo ambaye yupo hai mahali fulani…Na sidhani kama mpinga-Kristo atafunuliwa ila mpaka baada ya wakati wa kunyakuliwa. Kwa hivyo, hawa watu wote wanaojaribu kujua yeye ni nani, mimi huwa ninasema hivi kila wakati: ikiwa utakuja kufahamu yeye ni nani, basi nina habari

> mbaya kwako. Umewachwa nyuma.
>
> Hull: (Anacheka) Usifikirie mpinga-Kristo ni nani, fikiria Kristo ni nani, hadi unyakuzi ufanyike.

Hatua hii inafichua unyakuo wa siri na kalenda ya matukio inayokuja nayo kuwa ni udanganyifu wa hali ya juu. Haishangazi, wanatheolojia waprotestanti hawakuwa wa kwanza kudai kuwa utambulisho wa mpinga-Kristo hautajulikana mpaka wakati fulani ujao. Chimbuko la msimamo huu linaanzia wakati wa makabiliano wa mageuzi ya kanisa (counter-reformation) ya karne ya 16.

Mara tu baada ya kujitenga na Rumi (Rome), wanamageuzi hao walijibidiisha kutafsiri zaidi ya alama 20+ za kumtambulisha mpinga-Kristo zinazo patikana kwenye Maandiko. Hilo liliwafanya wakafikia hitimisho kwa kauli moja kuwa msimamizi wa Kanisa Katoliki, yaani Papa ndiye aliyehusika kama mpinga Kristo. Martin Luther alitangaza:

> Hatimaye ninajua kuwa papa ni mpinga Kristo, na kwamba kiti chake cha enzi ni cha Shetani mwenyewe. — D'Aubigne, b. 6, sura ya 9. GC 141.3.

Baada ya kugunduliwa, wasomi wa Rumi walianza kuzifanyia kazi mbinu za kubadilisha mambo. Kwa kuwa Biblia ilimtaja kwa uwazi sana yeye kuwa ni mfumo wa mpinga-Kristo, njia pekee iliyowezekana ya kusitisha tafsiri ya waprotestanti ilikuwa ni kugeuza kibao cha mpinga-Kristo kwenye siku hizo.

Hapo awali, wasomi wa Rumi wakaanza kuandika vitabu vingi vya wasomi wanaohesabu muda wa utawala wa mpinga-Kristo—kabla ya kanisa kuanza kutawala—au wangemuweka kwenye siku zijazo za mbali. Mwanamatengenezo anayeitwa Thomas Brightman (1562-1607) alitumia hila hii ya kukatisha tamaa:

> Nyakati fulani hawakumruhusu mtu yeyote aguse Biblia, sasa wanatoa maelezo ya kuifafanua—kuwafanya watu wawe na mawazo ya mbali juu ya Papa Mpinga Kristo.

Hapo awali, kasisi Mjesuiti wa Uhispania anayeitwa Luis De Alcazar (1554-1613) alianzisha wazo la kuuweka unabii wote nyuma. Alcazar aliuweka utawala wa mpinga-Kristo kabla ya Kanisa Katoliki kutawala, akimtambulisha kuwa Mfalme Nero. Hata akadai kuwa kilichomuangusha mpinga-Kristo ilikuwa ni kuinuka kwa Kanisa Katoliki, na kuwa ndipo chanzo cha ufalme wa Kristo uliotajwa kwenye Ufunuo. Kitabu cha Alcazar kinachojulikana kama preterism kilichapishwa kikiwa na kurasa 900 baada ya kifo chake mwaka 1614.


Licha ya madai ya kuwa kanisa Katoliki ndilo lisilokosea kuitafsiri Biblia, ndugu mmoja wa Alcazar alikuwa amechapisha msimamo ulio kinyume kabisa kwa kipindi cha chini ya robo ya karne moja hapo kabla. Na kama tutakavyoona, wale wanaoamini mambo ya unyakuo wa siri wamebuni mafundisho yao kwenye msingi huu.

## MISINGI YA FUTURISM

Kasisi anayeitwa Francisco Ribera aliongoza harakati za misingi ya Futurism. Alijaribu kumficha mpinga-Kristo wa kweli kwa kudai kuwa unabii wote unaomhusu ungetimizwa nyakati fulani kwenye wakati ujao wa mbali.


Kwenye jaribio dogo sana la kutoa uthibitisho wa hesabu yake, Ribera alikisia kuwa kulikuwa na pengo kubwa kati ya juma la 69 na la 70 kwenye unabii wa majuma 70 wa Danieli 9.

Kwa kuzingatia kanuni ya siku kwa mwaka ya wakati wa kinabii (Ezekeli 4:6), wiki ya siku 7 inawakilisha miaka 7 halisi. Wiki ya 70 ilianza na ubatizo wa Kristo mwaka 27 BK na ilikamilika mwaka 34 BK kwa kupigwa mawe Stefano.




Lakini Ribera, kwa hila, aliliondoa juma la mwisho kutoka kwenye unabii uliosalia na kudai kuwa kipindi hiki cha mwisho cha miaka saba kingeanza wakati wa mpinga-Kristo, na kuwa ilikuwa ni mbali sana kwenye siku zijazo ambazo ni za mbali.

Kwa kuitenga miaka saba ya mwishoni, Ribera anaharibu utabiri wa kustaajabisha unaoashiria ubatizo na kusulubishwa kwa Kristo. Hii ni mbaya zaidi kuliko ukosefu wa uaminifu akilini, kwani inampa mpinga Kristo kile kinachomilikiwa na Mwokozi.




Tazama tena jinsi Dkt. Mark Hitchcock anavyobadilisha tarehe, akijaribu kukifanya waziwazi kile kilichofanywa na Jesuit:

> Kwa hiyo, unabii huu unatimizwa hadi leo hii. Ni unabii mkubwa zaidi kwenye Biblia. Sasa hizo ni wiki 69 za kwanza za miaka. Kwa hivyo tunaanzia hapa kushoto: Machi 5, 444 KK. Hayo majuma 69 ya kwanza ya miaka yanafanya unaifikia Machi 30, BK 33; kuingia kwa Yesu kwa ushindi. Kwa hivyo, wiki moja ya miaka bado ipo. Lakini kabla ya kipindi hicho cha miaka saba kuanza kuna muingiliano, kuna muda usiojulikana ambao tunaupata katika mstari wa 26…pengo lililopo kati ya mwisho wa ile ya 69 na mwanzo wa juma hilo la mwisho.

Msingi wa Futurism wa Ribera unaweza kuwa umechukua mamia ya miaka ili kulifikia lengo lililotarajiwa, lakini ole! Maadui wa zamani wa Rumi siyo tu wameikubali, lakini wamegeuzwa kuwa washirika wake wenye nguvu sana.

Futurism ya Ribera ilianza kuingia katika makanisa ya kiprotestanti mapema kwenye karne ya 19 wakati watu wanaopinga matengenezo ya kanisa nchini Uingereza walipoanza kutangaza hila ya zamani ya jesuit ya mpinga-Kristo wa siku zijazo.

Mwanatheolojia wa Kiingereza anayeitwa Nelson Darby alikuwa ni mtu mashuhuri aliyezingatia imani ya Ribera ya Futurism. Kufikia mwaka 1835, Darby alikuwa ameunganisha tafsiri hii ya kinabii na 'kunyakuliwa kwa siri'. Kisha akasafiri nje ya nchi akitangaza mafundisho yake.

Fundisho hili la kuficha mpinga-Kristo leo limepambwa kwa wito wa kiinjilisti kama ambavyo John Macarthur anavyofafanua:

> Wakati wa kipindi cha dhiki, uamsho mkubwa zaidi kwenye historia ya mwanadamu unafanyika. Una watu wengi waliookoka kwenye kipindi cha miaka saba kuliko wakati mwingine wowote kwenye historia na hiyo imewekwa wazi sana kwenye Maandiko. Kimsingi, taifa zima la Israeli huja kwa imani kwa Kristo. Waasi wanaondolewa na hatimaye Israeli inamkumbatia Yesu Kristo kama Masihi, wanamtazama Yeye ambaye walimuumiza na kadhalika.

Kadri uamsho kama huo unavyosikika, muundo huu wa kinabii ni mageuzi ya theolojia ya kupinga urekebishaji wa ile ya Ribera, ambayo inapambwa kumfanya mpinga-Kristo wa kweli asionekane. Tazama tena jinsi ambavyo Mchungaji John Hitchcock anadai kuwa hatuwezi kujua ni nani ambaye ni Mpinga Kristo:

> Biblia inazungumza kuhusu mtawala huyu wa ulimwenguni ajaye: mpinga-Kristo. Inavutia kuona anaitwa ni mhusika mwenye pembe ndogo. Kwa hivyo, anajitokeza kwanza akiwa haeleweki. Ndiyo maana kila mara watu wanaponiandikia na kusema, je, unafikiri mpinga-Kristo ni nani, na unajua wanajaribu kumtambua mpin-

ga-Kristo. Hatujui yeye ni nani hadi leo. Ataibuka bila ya kuelewe-ka. Kama mtu atatokea kwa kueleweka leo hii basi huyo siyo yeye.

Lakini baada ya hayo yote, Hitchcock anakiri kuwa nambari ya jina ya mpinga Kristo ni 666:

> Alama ya mnyama ni 666 pale kwenye kitabu cha Ufunuo. Lakini ninadhani kwa ufasaha kuwa itakuwa ni tarakimu ya namba ya jina lake. Kwa maneno mengine, kama kwenye lugha ya Kigiriki na Kiebrania, unaweza kuzichukua herufi za alfabeti, zina thamani ya namba. Na hivyo unaweza kuchukua jina la mtu na kweli ukatoka na namba inayowakilisha jina hilo. Kwa hivyo, ninadhani jina lake litakuwa sawa na 666. Hivyo ndivyo atakavyotambulika.

Lingekuwa jambo la kushangaza kama Hitchcock asingejaribu kuonesha njia yake yeye mwenyewe juu ya mpinga-Kristo wa jadi: Papa. Kulingana na 'Decretum of Gratian' (kanuni ya karne ya 12 ya sheria ya kikanisa), jina rasmi la Papa ni 'Vicarius Filii Dei', linalomaanisha: Vicar of the Son of God (Mshirika wa Mtoto wa Mungu). Pia, inashuhudiwa na mashahidi wengi kuwa siku ya matukio Papa huvaa tiara yenye maandishi sawa na hayo, na kuwa imeandikwa juu ya mlango wa Vatican (tazama Facts of Faith kilichoandikwa na Chrstian Edwardson kwa ajili ya kuyafahamu mambo hayo).

Kwa kuona kuwa Kilatini ndiyo lugha rasmi ya kanisa, tunaweza kuhitimisha kuwa hiki ndicho cheo rasmi cha Papa. Tafadhali angalia jumla ya herufi hizi za Kilatini hapa chini:

## Vicarius Filii Dei

*(Vicar wa Mtoto wa Mungu)*

| | | |
|---|---|---|
| V = 5 | F = 0 | D = 500 |
| I = 1 | I = 1 | E = 0 |
| C = 100 | L = 50 | I = 1 |
| A = 0 | I = 1 | 501 |
| R = 0 | I = 1 | |
| I = 1 | 53 | |
| U = 5 | | |
| S = 0 | | |
| 112 | | |

= 666



Pamoja na yote yaliyosemwa, Yesu alimaanisha nini kwenye Mathayo 24 Alipozungumza juu ya mmoja kuchukuliwa, na mwingine kuachwa? Hiki ndicho kifungu cha msingi—pamoja na ulinganifu wake kwenye Kitabu cha Luka—ambacho kinatumika katika kufundisha unyakuo wa siri.

> Mathayo 24:40 Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa.
> 24:41 wanawake wawili watakuwa wakisaga; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa.

Kwa kuanza, tuchunguze muktadha wa mistari hii miwili kwenye Mathayo 24. Wazo linaanza na tangazo kuwa hakuna mtu ajuaye siku au saa hususani ya kuja kwa Kristo. Kisha Yesu anatukumbusha yale yaliyowapata wale waliotangulia:

> Mathayo 24:37 Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.
> 24:38 Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina,
> 24:39 wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.

Ni roho ya kupenda anasa za ulimwengu ambayo inawafanya watu kuwa vipofu juu ya uharibifu unaokuja. Hapa Yesu anatukumbusha kuwa ilikuwa ni kupenda mambo ya ulimwengu ambayo ilisababisha watu kukataa wokovu uliyotolewa kupitia safina.

Baada ya kutoa ulinganifu huo, Yesu anatoa mfano wa wale wanawake wawili kwenye mawe ya kusagia.

> Mathayo 24:40 Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa.
> 24:41 wanawake wawili watakuwa wakisaga; mmoja atwaliwa, mmoja aachwa.
> 24:42 Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja

Bwana wenu.

Uwiano kati ya siku za Nuhu na siku za mwisho upo wazi. Wale waliokubali wito wa Nuhu waliingia ndani ya safina na kuokolewa, lakini wale waliokataa waliwachwa nje. Hawakupata nafasi ya pili, na walizamishwa na mafuriko.

Vivyo hivyo, mwanamke anayechukuliwa anafananishwa na wale wanaokwenda mbinguni pamoja na Yesu kule mwisho wa dunia. Wakati mwanamke aliyeachwa nyuma anawawakilisha wale ambao wameachwa kwenye uharibifu, kama vile wenye dhihaka waliokufa kwa gharika.

Kwa wasiyo sikiliza injili, Bwana wetu atakuja kama mwizi usiku. Ni waovu, wala si watakatifu, ndiyo watakaonaswa, kama mtume Paulo asemavyo:

> 1 Wathesalonike 5:2 Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku.
> 5:3 Wakati wasemapo, Kuna amani na salama; ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafula, kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa.

Mwenye dharau, mwenye kupenda anasa atakabiliwa na uharibifu wa ghafla. Lakini Paulo haishii hapo. Ingawa hakuna mtu awezaye kutabiri siku au saa, Paulo anaweka wazi kuwa waaminifu hawatapatwa gafla bali watazidi kukesha. Tofauti kabisa na mtu anayeibiwa akiwa amelala, Paulo anatangaza haya kwa wenye haki:

> 1 Wathesalonike 5:4 Bali ninyi, ndugu, hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi.

Matone makubwa ya mvua yalipoanza kunyesha juu ya safina, Nuhu hakushangaa. Akiwa na ubao, misumari na maombi, alikuwa amejitayarisha kwa tukio hili kwa muda wa miaka 120. Vivyo hivyo, watu wa Mungu watakuwa wanautazamia ujio wa pili wa Kristo, kama yafunuliwavyo kwenye Mathayo 24. Yesu hatakuja kama mwizi usiku kwa wale

ambao wametii kutimia kwa unabii wa Biblia kwa unyenyekevu.

Lakini unyakuo wa siri unafundisha kwamba kazi kubwa ya uinjilisti itafanywa baada ya watakatifu kuondolewa kwa siri. Ikimaanisha kuwa wale watakaokosa unyakuo watapata fursa ya pili.

Hata hivyo, wale waliofungiwa nje ya safina hawakupata nafasi ya pili, bila kuwa na nafasi iliyosalia ya kutubu. Na ndivyo itakavyokuwa kwa wale wanaopuuzia fursa za kutoka mbinguni za kujifunza ukweli. Kama yule mwanamke aliyeachwa nyuma kwenye mfano wa Kristo, siku inakaribia ambapo rehema itafungwa milele juu ya ulimwengu usiojihadhari.

Imedhihirika kuwa inahitajika nguvu kidogo sana kuwashawishi walimwengu kupokea kile ambacho hawakitamani, wala kujali kuzitambua athari zake. Biblia inaonya vikali kuhusu agizo la wakati ujao:

> Ufunuo 14:9 ... Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake,
> 14:10 yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo.

Ulimwengu wote utamsujudu huyo mnyama kwa kupokea chapa yake:

> Ufunuo 13:3 Nikaona kimoja cha vichwa vyake kana kwamba kimetiwa jeraha la mauti, na pigo lake la mauti likapona; Dunia yote ikamstaajabia mnyama yule.
> 13:4 Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?

Mara tu mtu anapoipokea alama hii, hakuna kurudi nyuma. Baada ya hapo ulimwengu wote bila ya huruma utakubali mamlaka ya laana ya

milele ya mamlaka za ulimwenguni.

> Ufunuo 13:16 Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao;

Ili tuiepuke ile chapa inayokuja upesi ya yule mnyama tunapaswa kwanza kujua mnyama huyo ni nani.

Kwa maelezo kamili ya mnyama na alama yake, tafadhali angalia semina yetu ya unabii: *Maono ya 2020: Kufunua Alama ya Mnyama (2020 Vision: Unveiling the Mark of the Beast)*.

Jambo la kushangaza, John Macarthur na huduma yake ya *Grace to You* ni miongoni mwa waendelezaji wa udanganyifu wa kukabiliana na mageuzi ya Ribera. Na tena, wao wanasifu kazi ya Luther na warekebishaji wa kanisa la Protestanti, wakisema kwenye nukuu hii: "Isingekuwa kazi ya watumishi hao waaminifu, bado tungekuwa tunaishi chini ya utawala wa giza wa uongo wa Kikatoliki hadi hii leo".

Inashangaza sana kuwa wahudumu hawa, kinyume cha moja kwa moja na watumishi wanaowaita waaminifu, wanajishughulisha na kuendeleza uongo mbaya zaidi wa kupinga matengenezo!

Kwa hakika, theolojia ya unyakuo wa siri imewatia upofu wafuasi wao wasijue utambulisho wa adui yao, ambaye amewashika mkono anawaongoza kwenda juu ya mteremko mkali wa kuangamia milele.

> Ufunuo 13:4 Wakamsujudu yule joka kwa sababu alimpa huyo mnyama uwezo wake; nao wakamsujudu yule mnyama, wakisema, Ni nani afananaye na mnyama huyu? Tena ni nani awezaye kufanya vita naye?

**Kwa taarifa zaidi:**
www.earthenvessels.org.au



Unyakuzi wa siri upo kwenye Biblia? Ni hatari gani zinazompata Mkristo anayeshikilia msimamo huu?

Ukifuatilia fundisho hili na kurudi kwenye asili yake ya kupinga urekebishaji wa kanisa, utagundua ni nini, au nani aliyekusudiwa kufichwa na mafundisho hayo.

EARTHEN VESSELS

2 CORINTHIANS 4:7